

Je,
Adhabu ya
viboko
ina madhara
gani?

B C

3

Viboko
havikubaliki
hana!

Jishindie kompyuta
ndanil.

Adhabu ya kuchapa wanafunzi ni:

Adhabu yoyote inayosababisha
maumivu ya kimwili.



Kuchapa kwa
mikono, vitu,
kupiga teke,
kuunguza,
kusukuma,
kufinya,
nk.

Vilevile ni adhabu
yoyote ile isiyo ya
kimwili ambayo
hudhalilisha,
hutishia, huogopesha
na humuaibisha
mtoto.





Asilimia 98 ya
watoto wamedai
kuwa
wameshakumbwa
na adhabu hii...



Mtoto mmoja kati
ya watatu
hukumbwa na
adhabu hii
kila wiki.

Kwahiyo? Jambo hili lina ubaya gani?

Ni jambo ambalo tumekuwa
nalo, hivyo tunadhani ni
jambo zuri kwa malezi ya
watoto wetu!



Wala
hatuwaumizi
watoto wetu!

Kweli!
Tunawashikisha
adabu!



Lakini adhabu ya kuchapa wi



anafunzi ina madhara mengi!



Madhara ya kimwili

Ninapaswa nichote maji na
kusafisha nyumba kabla ya kwenda
shule. Mara nyingi ninachelewa
kufika shulen!



Mara nyingi ninachapwa ninapochelewa.
Siku moja nilijificha kichakani mpaka
mwisho wa vipindi.



Mwalimu alinikamata na akakasirika sana!
Alinichapa viboko 20!



Alinichapa sana nikaumia, wazazi wangu
wakanipeleka hospitali na nilishindwa kwenda
shule wiki nzima.



Maumivu ya hisia



Naona unataka kujifunza kufua! Sasa,
nenda nyumbani kwa matroni ukafue
nguo zake zote...



Na ndiyo maana
umefeli mtihani
wa hisabati,
mjinga wewe!

Hakuna anayenijali! Sijui maisha
yangu yatakuwaje!



Inaniumiza
rohoni!

Madhara ya kitabia



Baadaye siku hiyo...



Madhara ya kimahusiano

Hassan, funga domo
lako! Na uache kusukuma
kiti cha Hasifa!



Hassan, inatosha! Sasa
ngoja nikufundishe
adabu! Hebu peleka
tofali 100 kule kilimani!



Namchukia! Na
nitaendelea
kumchokoza kila
siku!



Wiki iliyofuata...



Ugumu wa kujifunza



Hivi hili darasa lina
tatizo gani? Ni mara
ngapi nimefundisha
jambo hili?

Fatima, njoo hapa!
Sasa ninawashikisha
adabu muwe wasikivu!





WIKI ILIYOFUATA



We binti mjinga! Unajua kuwa
nitakuchapa, na bado hutaki kujibu!



Najua hali hii
itaendelea kutokea,
sijui nifanyeje?

Inanifanya
nishindwe kujifunza.
Ninajihisi mjinga





Adhabu ya kupigwa
huwafanya watoto
kujisikia vibaya...Lakini
bado watu wazima
wanatoa sababu za
kuendelea kutumia
adhabu hii.

Kama mtoto hakuogopi, kamwe hatakuheshimu!



Mshenzi wewe! Jifunze kuheshimu wakubwa!



Lakini huwezi kumlazimisha mtu kukuheshimu!

Hicho kichapo kitakufanya uniheshimu!



Heshimu watu! Watakuheshimu pia!



Mwalimu mzuri ni yule anayedhibiti tabia ya mwanafunzi.

Sababu
2



Nani anapiga kelele? Ninasikia kelele mpaka ofisini kwangu!

Siyo mimi!

Sielewi somo!


Kimya!

Wanafunzi huweza kukaa kimya kwa kuogopa adhabu...

Mara vitisho vinapoondoka



Matokeo ya nidhamu ya woga...



Walimu wazuri hawadhibiti tabia za wanafunzi kwa kuwachapa au kuwatukana.



**Huwezi kudhibiti ubunifu...
bali unaweza kuchochea tu!**

Nilikuwa nikichapwa na imenifunza
nidhamu nzuri!

Sababu
3



ZAMANI:



Hutoweza kuelewa
sayansi, mjinga
wewe!

SASA:



Mimi
mwenyewe
sikuelewa
sayansi, wewe
mjinga ndo
utaelewa!

Lakini...

Jaribu kuwaza jinsi ambavyo mafanikio yako yangeweza kuwa!



Lakini mchelea mwana kulia, hulia
mwenyewe!



Mithali ya biblia
kuhusu viboko
ilikuwa kwa nyakati
zile...

Lakini, Agano
Jipya husisitiza
upendo na
msamaha





Viboko ni mila na desturi zetu! Hatutaki
kukumbatia maadili ya nje!

Sababu
5



Lakini mila na
desturi zetu SIYO
kuumiza watoto!

Huzingatia
heshima, upendo
na maelekezo



Tunataka watoto
wetu wakue na
kupenda
mapokeo yao...

...sio
kuyaogopa!



Mtaka cha uvunguni sharti ainame!



Wanafunzi wangu wamefaulu
mtihani kwa sababu waliweza
kukariri kila kitu kwasababu
ya kuogopa viboko!

Kweli? Hivi
kweli
wanaelewa?



Salma, jana ulikariri namna ya kukokotoa hesabu ya eneo la mstatiri. Sasa namna gani unaweza kukokotoa eneo la mcheduara?



Kujifunza kwa
viboko kunatulazimu
kukariri!

Kweli, hatujifunzi
namna ya kufikiri!

Tumekuwa
wanafunzi
mbumbumbu!



Lakini tunatumia adhabu ya viboko
kidogo tu inapobidi!



Jaribu kufikiria iwapo bosi
wako atakuchapa kofi, hata
mara moja tu, kwa kuchelewa
kumaliza ripoti. Utajisikiaje?



Ninatumia adhabu ya viboko pale
inaponilazimu tu!



Aah...nimesahau
homuweki yangu!

Duh! Pole sana
Saad, leo
utalambwa viboko!



Hapana, mwalimu
hatanichapa ataniamini.

Saad! Umesahau homuweki yako!
Hakuna njia nyingine ya kukumbusha!

Lakini nilikuamini!
Ulisema
hutatuchapa!
Sikuelewi!



Alaa! Kumbe adhabu ya
kumtandika mwanafunzi
hudhoofisha kujiamini
kwake!



Kila mmoja anakubali,
adhabu ya viboko haisaidii!




**Ulimwenguni kote, watu
wameamua kuachana na
adhabu ya kuchapa
wanafunzi!**



Sera za kimataifa zinaeleza kuhusu maamuzi hayo ya dhati




Sera ya Afrika pia huzungumza kuhusu maamuzi haya thabiti.




Sera ya Tanzania ina mkanganyiko





Licha ya kuridhia mikataba ya kimataifa ya haki za watoto, Tanzania bado inatumia adhabu hii!
Waraka huu unapingana na Katiba na sera ya mtoto.

**Shule nzuri
huzingatia sera za
kimataifa, kitaifa na
kikanda.**



**Shule nzuri
huunda sera
inayopinga
adhabu ya
viboko kwa
wanafunzi.**

Katika shule

Ninajisikia
huru na
ninalindwa!

Ninajifunza
vizuri bila
woga!

Ninaheshimiwa
na ninaheshimu
pia!



Shule nzuri HAINA adhabu ya kuchapa war

nzuri...





Je, unaweza kufanya nini kuhusu
adhabu ya kuchapa wanafunzi?

- Amua kuachana na adhabu hii kwa kudhamiria moyoni.
- Jenga mazingira ya kuepuka adhabu hii shulenii.
- Jifunze kuhusu nidhamu isiyo ya uoga na kisha tumia mbinu za kusisitiza nidhamu hiyo.
- Wasikilize wanafunzi na kutatua matatizo yao.
- Jadili na watu wengine kuhusu faida za utulivu.
- Kuwa mbunifu! Jaribu kutumia mbinu mpya darasani.

Jinsi ya kutumia kijitabu hiki...

- Soma kijitabu hiki pamoja na wanafunzi au walimu wengine. Kisha jadilini madhara ya adhabu ya viboko.
- Fanya utafiti kuhusu sheria na sera zinazoongoza shule, wilaya, mkoa na nchi nzima kwa ujumla. Jadili undani wa sheria na sera hizo.
- Fanya mijadala ukitumia sababu watu wanazotoa kuhusu kuendelea kutoa adhabu hii na kisha fafanua madhara yake.
- Fanya maigizo kuhusu adhabu hii na kisha onesha jinsi watoto wanavyoadhirika kutokana na adhabu hii.
- Shirikisha familia yako kujua athari za adhabu hii.
- Tumia sera zinazopaswa kuzingatiwa ili shule iwe nzuri.

Toa maoni, shiriki na

Msomaji, Serikali yako inataka kukusikia! Shiriki kwa kutuma maoni yako. Mawazo yako yanaweza kuboresha huduma kwa jamii na utawala bora. Pia, hii itakuza ushirikiano katika ya wananchi na Serikali. Maoni yako yatahusiana na **mafunzo** uliyopata kupitilia kitabu hiki. Kigezo cha kupata washindi ni ubunifu au wazo jipya.



Zawadi:



Kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka 2012, maoni ya wanafunzi yatakayotumwa kuititia shule zao yatashindanishwa. Maoni kumi bora yatachaguliwa na yatachapishwa kwenye vitabu pamoja na tovuti. Kila shule itakayoshinda itapata kompyuta ndogo mbili (laptops).

jishindie kompyuta!

Mwisho wa maoni yako weka taarifa zako:



- a) Tarehe
- b) Majina kamili, umri wako na jina la shule/taasisi
- c) Jinsia - Mwanaume/Mwanamke
- d) Anuani (SLP) kamili, makazi (Kata, Wilaya, na Mkoa)
- e) Simu yako na/au Barua pepe (kama unayo).



Unangoja nini! Shiriki basi kwa njia zifuatazo.
Tuma kwa:



- Barua: OGP Ikulu, S.L.P 9120 Dar es Salaam
- Barua pepe: ogp@ikulu.go.tz au opengovtz@gmail.com
- Tovuti: www.wananchi.go.tz

Fikiria. Paza Sauti. Twaweza!

Kuthaminiwa
zaidi!

Kitabu hiki kimeandaliwa na:



Viboko
havifai!

Jadili na wenzio ulichojifunza humu
au shiriki mjadala kuitia:



Twaweza_Nisisi



Twaweza Tanzania

www.twaweza.org
www.raisingvoices.org